# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
# NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
# CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

)15/2

## ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 2
## (Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**/IUDA: Saa 2 Dakika 30** **2006/10/16 Mchana**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C na D.
2. Jibu maswali **manne (4),** swali **moja (1)** kutok ... .emu.
3. Kila swali lina alama 25.
4. Mashine za hesabu za elektroniki **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 2 zenye maandishi.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## BISMILLAHIR - RAHMANIR - RAHIIM

## SEHEMU A - QUR'AN

1. "Tuongoze njia iliyonyooka, njia ya wale uliowaneemesha, siyo ya wale waliokasirikiwa wala ya wale waliopotea (1 : 6 - 7)". Bainisha watu waliopotea na sababu zilizowafanya wawe hivyo.

2. Hatukuiteremsha hii Qur'an ili upate mashaka (20 : 2). Pamoja na ahadi hii ya Mwenyezi Mungu, kwanini Waislamu leo wanaishi katika maisha ya mashaka?

3. Nadharia ya makafiri wa leo wanadai kuwa Qur'an ameitunga Muhammad kwa sababu za kiuchumi. Je unakubaliana na maelezo hayo? Toa sababu zako.

## SEHEMU B -TAWHIID

4. Chambua madai ya makafiri yanayosema Mungu hayupo kwa sababu haonekani.

5. Eleza kwa kina maana ya kumuamini Mwenyezi Mungu.

6. Onesha udhaifu wa sababu za makafiri zinazowapelekea kukanusha kuwepo kwa maisha baada ya kufa.

## SEHEMU C - FIQH

7. Eleza matatizo yaliyojitokeza katika kukua kwa sayansi ya Fiqh na Fiqh.

8. Taja mambo yaliyosababisha kuharamishwa kwa riba katika mfumo wa maisha ya kiuchumi wa Kiislamu.

9. "Na kama ukiogopa kutowafanyia uadilifu mayatima, basi oeni mnaowapenda katika wanawake wawili au watatu au wanne ------ (4 : 3)". Onesha kuwa, ruhusa ya kuoa wake wengi haiongezi kasi ya kuenea kwa ukimwi kama wanavyodai wahudumu wa ukimwi.

## SEHEMU D - TAREKH

10. Eleza vyanzo vya vikwazo vya kusimamisha Uislamu nchini Tanzania.

11. Eleza ni mambo gani Waislamu wa leo tunajifunza kutokana na mateso waliyopata Waislamu wa wakati wa Mtume (S.A.W).

12. Eleza jinsi Makka ilivyokombolewa na kusimama kwa Uislamu wakati wa Mtume.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org